

**A WAGALATIA WAPUMBAVU. Wagalatia 3:1-5.**

- ❖ Paulo anatumia manemo makali na ya wazi kuwafanya wagalatia watazame waliposimama.
- ❖ Walikuwa wamempokea Yesu kwa imani, lakini wakawa wakiondoa haki ya Yesu na badala yake kuweka matendo yao ya sheria.

**B IMANI YA AGANO LA KALE. Wagalatia 3:6-8.****❖ MAMLAKA YA AGANO LA KALE.**

- Maandiko—huhusisha agano jipya—ni mamlaka kuu ya mafundisha.
- Thiologia ya Paulo imejikita katika nukuu za Biblia. Tunaweza kuzipata nukuu hizo kwenye nyaraka zake hata kwenye zili fupi kabisa, Tito na Filemoni.

**❖ KUHESABIWA HAKI KATIKA AGANO LA KALE.**

- Wayahudi waliamini kuwa Mungu alimbariki Ibrahimu na uzao wake kwa sababu ya utii wake mkamilifu.
- Hata hivyo, Paulo anatumia mfano wa Ibrahimu kuelezea kinyume cha hicho. Je; Ibrahimu alikuwa mwenye haki kwa sababu ya utii wake? Kwa hakika hapana.
- *His Imani yake ilipata thawabu ya haki, na si matendo yake.*
- Hakufanya matendo hayo ili ahesabiwe haki, bali kwa sababu tayari alikuwa amekwishahesabiwa.

**❖ INJILI KATIKA YA AGANO LA KALE.**

- Mungu alifundisha injili kwa Ibrahimu. Mungu alimuahidi Ibrahimu familia kubwa na mahali pa kuishi. Zaidi ya hayo, Alimfundisha kuwa Masihi atatoka katika uzao wake na ataifia kila dhambi (Mwanzo 22:1-18).
- Ibrahimu hakuambiwa aahidi chochote. Alipaswa kukubali ahadi za Mungu. Hakukuwa na tendo lolote Ibrahimu alilipaswa kufanya ili apokee hizo ahadi.
- Daudi na Yohana ni mifano miwili kutoka katika agano la kale ya msamaha kwa njia ya toba na si matendo (Zaburi 32:1-5; Zakaria 3:1-4).

**C KUOKOLEWA NA LAANA YA DHAMBI. Wagalatia 3:10-14.**

- ❖ Kanuni ni rahisi. Kama ukitii, basi utabarikiwa. Kama ukiasi katika moja, utalaaniwa (Kumb. 27 na 28). Ni aidha yote au Hakuna kitu kabisa.
- ❖ Kwa kuwa wote tumetenda dhambi (Warumi 3:23), wote tu chini ya laana ya dhambi.
- ❖ Lakini Kristo alitukomboa. yaani, alitununua kwa kulipa fidia yetu. Alibeba laana na adhabu ya dhambi zetu kwa kufa msalabani (Yohana 3:16; 1 Wakorintho 6:20; 2 Wakorintho 5:21).
- ❖ Kila anayeshiriki Imani ya Ibrahimu anaweza kupata zawadi hiyo.